

Taarifa. Aidha, endapo mhusika wa taarifa ambaye ridhaa yake inaombwa atakuwa ni mtoto, mtu asiye na akili timamu au mtu mwingine asiye na uwezo wa kutoa ridhaa, ridhaa ya mtu huyo itapatikana kutoka kwa mzazi, mlezi, mrithi, wakili au mtu mwingine yeyote anayetambulika kisheria.

## TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

Kwa Maoni, wasiliana na Tume  
kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,  
Tume ya kurekebisha Sheria  
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,  
Barabara ya Mkalama  
S.L. P 1718  
DODOMA  
TANZANIA

Barua pepe: [lrct@lrct.go.tz](mailto:lrct@lrct.go.tz)  
Tovuti: [www.lrct.go.tz](http://www.lrct.go.tz)



## SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI



### Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

### Taarifa Binafsi

Taarifa binafsi ni taarifa yoyote ambayo inaweza kutumika kumtambua mtu mahsusi. Kwa mfano, jina kamili, anwani, tarehe ya kuzaliwa, namba ya hati ya kusafiria na namba ya leseni ya udereva.

Taarifa binafsi nyeti ni taarifa yoyote ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi inachukuliwa kama ina athari kubwa katika haki na maslahi ya mhusika wa taarifa. Taarifa hizi zinajumuisha taarifa za vinasaba, taarifa za watoto, taarifa zinazohusu miamala ya kifedha ya mtu binafsi, taarifa za kibayometriki, taarifa za kiafya n.k.

### Malengo ya Sheria

Sheria ina lenga kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi na kumairisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na binafsi.

### Umuhimu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44

- Kudhibiti ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi.
- Kuhakikisha ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi unafanyika kwa kuzingatia misingi ya Sheria.
- Kulinda faragha za watu.
- Kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa kulinda taarifa binafsi.

### Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

Mkusanyaji au mchakataji wa taarifa binafsi anatakiwa kuhakikisha taarifa binafsi-  
• zinachakatwa kihalali, kwa haki na uwazi.  
• zinakusanywa kwa madhumuni mahsusi.  
• zinatoshleza na ni muhimu kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

- ni sahihi, zinaboreshwa, zinahakikishwa na kurekebishwa inapobidi.
- zinahifadhiwa kwa namna inayoruhusu utambuzi wa mhusika wa taarifa kwa muda ulioanishwa kisheria.
- zinachakatwa kwa kuzingatia haki za mhusika wa taarifa.
- zinachakatwa kwa kuzingatia usalama wa taarifa binafsi.
- hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume na masharti ya sheria.

### Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

Tume ina majukumu yafuatayo;  
• Kufuatilia utekelezaji wa Sheria kwa wakusanyaji na wachakataji taarifa.  
• Kusajili wakusanyaji na wachakataji taarifa.  
• Kupokea, kuchunguza na kushughulikia

malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa na faragha za watu.

- Kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu.
- Kutoa elimu kwa umma kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi.
- Kufanya utafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa.
- Kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi.
- Kuishauri Serikali masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

### Makosa na Adhabu

Mtu ambaye ataharibu, atafuta, atapotosha, ataficha au kubadilisha taarifa binafsi kinyume cha sheria anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

### Hitimisho

Mtu yeyote haruhusiwi kuchakata taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi ya mhusika wa taarifa. Mhusika wa taarifa anaweza kuondoa ridhaa yake wakati wowote bila gharama wala maelezo yoyote. Hata hivyo, Waziri (mwenye dhamana ya masuala yamawasiliano) kwa kupitia kanuni anaweza kuamua mazingira ambayo katozo la uchakataji wa taarifa binafsi halitaweza kuondolewa hata kwa ridhaa ya mhusika wa